# Abortion / Kutoa Mimba ni Dhambi Kuu

Biblia inakiita kiumbe kilicho tumboni mwa mama yake "**mtoto**". Na adhabu inayotolewa ikiwa mtoto huyu atadhurika kwa uzembe na makusudi ya watu "utalipiza **uhai kwa uhai**". Yaani, kiumbe hiki kinazungumziwa kuwa ni "**hai**".

Ebu tusome aya kadhaa kutoka katika fasiri za Kiingereza za Biblia zenye mamlaka ya kuitwa "Biblia" na kisha tutaona tafsiri yake. Pia tutasoma kutoka "NEN Biblia" au "Kiswahili Contemporary Version" ambayo nayo ni fasiri nzuri pia ya Kiswahili.

{21:22} ***If men strive, and hurt a woman with child, so that her fruit depart [from her***,] and yet ***no mischief follow***: he shall be surely punished, according as the woman's husband will lay upon him; and he shall pay as the judges [determine.]
{21:23} And if [any] mischief follow, then thou shalt ***give life for life***,
{21:24} Eye for eye, tooth for tooth, hand for hand, foot for foot,
{21:25} Burning for burning, wound for wound, stripe for stripe.
(Exodus 21:22-25 King James Bible)

**22** ***If men who are fighting strike a pregnant woman and her child is born prematurely,*** but there is no further injury, he shall surely be fined as the woman's husband demands and as the court allows.
**23** But if a serious injury results, then ***you must require a life for a life***—
**24** eye for eye, tooth for tooth, f hand for hand, foot for foot,
**25** burn for burn, wound for wound, and stripe for stripe.
(Exodus 21:22-25 Berean Study Bible)

21:22 Ikiwa wanaume wawili wanapigana, wakamwumiza mwanamke mwenye mimba hata akajifungua kabla ya wakati, lakini asidhurike; sharti ataadhibiwa kama atakavyoandikiwa na mumewe huyo mwanamke; na atalipa kama waamuzi watakavyohukumu.
21:23 Lakini kama madhara yatatukia, ndipo ***utalipiza uhai kwa uhai***,
21:24 Jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu,
21:25 Kuteketeza kwa kuteketeza, jeraha kwa jeraha, chubuko kwa ajili ya chubuko.
(Kutoka 21:22-25 Tafsiri kutoka King James Bible na Berean Study Bible)

**22** Ikiwa watu wawili wanapigana na ***wakamuumiza mwanamke mjamzito, naye akazaa kabla ya wakati lakini hakuna majeraha makubwa***, mhalifu atatozwa mali kiasi cha madai ya mume wa yule mwanamke, na jinsi mahakama itakavyoamua.
**23** Lakini kukiwa na jeraha kubwa, ***ni lazima ulipe uhai kwa uhai***,
**24** jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu,
**25** kuchomwa moto kwa kuchomwa moto, jeraha kwa jeraha, mchubuko kwa mchubuko.
(Kutoka 21:22-25 NEN Biblia au Kiswahili Contemporary Version)

Kama kielelezo cha ukweli huu, Mungu anadhihirisha makusudi Yake kwa Esau na kwa Yakobo kabla hata hawajazaliwa. Soma:

**10** Wala si hivyo tu, bali pia watoto aliowazaa Rebeka walikuwa na baba huyo huyo mmoja, yaani, baba yetu Isaki.
**11** Lakini, **hata kabla hao mapacha hawajazaliwa** au kufanya jambo lolote jema au baya, ili kwamba kusudi la Mungu la kuchagua lipate kusimama,

**12** si kwa matendo, bali kwa yeye mwenye kuita, Rebeka aliambiwa, “Yule mkubwa atamtumikia yule mdogo.”
**13** Kama vile ilivyoandikwa, “Nimempenda Yakobo, lakini nimemchukia Esau.
(Warumi 9:10-13 NEN Biblia)

Mungu ndiye anayetuumba ndani ya tumbo la uzazi la mama zetu. Na kila kiumbe chake kina makusudi na malengo yake maalum. Soma:

**15**Je, yeye aliyeniumba tumboni mwa mama yangu,
si ndiye aliwaumba?
(Ayubu 31:15 NEN Biblia)

**5**“Kabla sijakuumba ndani ya tumbo la mama yako, nilikujua;
kabla hujazaliwa nilikutenga kwa kazi maalum;
nilikuweka uwe nabii kwa mataifa.”
(Yeremia 1:5 NEN Biblia)

**10**Nimekabidhiwa kwako tangu kuzaliwa,
toka tumboni mwa mama yangu
umekuwa Mungu wangu.
(Zaburi 22:10 NEN Biblia)

Watoto ni zawadi, tunu kuu kutoka kwa Bwana. Soma:

**3** Wana ni urithi utokao kwa BWANA,
watoto ni zawadi kutoka kwake.
**4** Kama mishale mikononi mwa shujaa
ndivyo walivyo wana awazaao mtu katika ujana wake.
**5** Heri mtu ambaye podo lake
limejazwa nao.
Hawataaibishwa wanaposhindana
na adui zao langoni.
(Zaburi 127:3-5)

Soma aya hizi kwa makini na utafakari. Mungu wetu anamchukulia kiumbe aliye tumboni mwa mama yake kuwa ni mwanadamu halisi mwenye kudura / hatma ambayo Yeye Mungu amekwishaipanga. Watu wengine hutoa visingizio kwamba kwa sababu ujauzito ulioko umetokana na ubakaji, incest (ngono baina ya maharimu – ndugu wa damu), “uwezekano” wa kuwa na ugonjwa wa kurithi kama sickle cell anaemia, nk kuwa ni sababu tosha ya kutoa ujauzito huo. Hii ni makosa. Kama Maandiko yanavyoonyesha, kila kiumbe kina makusudi yake katika mpango wa Mungu. Kazi yako ni kutimiza wajibu wako katika mnyororo huu wa uhai, basi. Mengine yote mwachie Yeye. Anajua nini anafanya. Na ikiwa utabeba “mizigo” basi jua thawabu yako I mkononi Mwake. Usitoe mimba! Wito kwa viongozi wetu: watawala na watungaji wa sheria – tujiepushe na kuhalalisha utoaji mimba, ili taifa letu lipate baraka za Mungu anayetoa neema kwa watenda mema

na laana kwa waovu! “Misaada” tunayopokea kutoka “nchi zilizoendelea” ni dalili ya laana kwa sababu ya kutokemea maovu na kutopambana na shetani.

Imeandikwa na Respicius Kilambo Luciani
https://sayuni.co.tz